

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 : Mwaka wa 1

Maswali

1. Kaini alifanya nini kujiendeleza maishani?
2. Habili alifanya nini kujiendeleza maishani?.
3. Kaini alimtolea Mungu nini?.
4. Habili alimtolea Mungu nini?.
5. Mungu alifurahia sadaka ya kaini ?.
6. Mungu alifurahia sadaka ya Habili?
7. Kaini alifanyaje Habili?
8. Mungu alimwambia nini Kaini?
9. Adhabu ya Kaini ilikuwa nini?.
10. Jina la mwana wa Adamu wa tatu aliitwa nani?

Majibu

1. Kaini alikuwa mkulima
2. Habili alichunga kondoo
3. Kaini alimtolea Mungu mboga
4. Habili alimtolea Mungu kondoo
5. Mungu hakufurahia sadaka ya kaini
6. Mungu alifurahia sadaka ya Habili
7. Kaini alimuuwa Habilil
8. Mungu alimwambia Kaini wapi ndugu yako , umemuuu
9. Kaini alifukuzwa na kuadhibiwa pekee yake.
10. Mwana wa Adamu wa tatu aliitwa Sethi

3 Kaini na Habili

Marejeo

Mwanzo 4

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tusifanye jambo lolote kwa njia zetu ila kwa njia ya Mungu. Lazima tusichukie wenzetu

Maneno maalum

1. Ngozi ya wanyama + dhambi + samehe + kifo cha mwana kondoo + kumwaga Damu + mwana kondoo wa Mungu
2. Mkulima + kondoo
3. Sadaka + mwana kondoo
4. Dhabihu + mboga
5. Kukubalika + ghadhabika(kasirika)
6. Kauwawa Habili
7. Wapi ndugu yako?
8. Kaini akalaaniwa
9. Fukuzwa
10. Sethi

3.1 Adamu na Hawa waliishi na furaha katika bustani hadi walipomuasi Mungu kwa kula tunda la ujuzi wa mema na mabaya. Kwa maana walitenda dhambi, waliadhibiwa na kufukuzwa kutoka kwa bustani.

Mungu alitengenezea Adamu na Hawa makoti (mavazi) ya ngozi ya wanyama ili wavae, walipotambua kwamba wako uchi na kuaibika. Hapa tunaonyeshwa kwamba dhambi inasamehewa tu kwa kifo cha mwana kondoo na kumwaga damu.

Hapa tunaelekezwa kwa kifo cha mwana kondoo wa Mungu, Yesu Kristo atakaeokoa ulimwengu.

3.2 Adamu na Hawa walikuwa na wana wakiume wawili, Kaini na Habili. Kaini alikuwa mkulima na Habili alichunga kondoo.

3.3 Walipokua wakubwa, walimletea Mungu sadaka. Kaini alileta matunda na mboga, lakini Habili alileta mwana kondoo.


3.4 Kaini na Habili walikuwa wamejua ya kwamba dhambi inasamehewa kwa kutoa mnyama, lakini Kaini alitaka kumtolea Mungu kwa vitu vyake mwenyewe. Hakutaka kununua mwana kondoo kutoka kwa Habili.

Alikataa mataakwa (hakujali) ya Mungu na akaleta matunda na mboga.



3.5 Mungu alikubali dhabihu ya Habili lakini hakufurahia vyenye Kaini alileta, Kaini alikasirika (gadhabika) sana alipoona Mungu amekataa matoleo yake.

3.6 Kaini alikasirika na akaenda shambani, kule alimpata Habili aliyekuwa akichunga kondoo wake, Kaini alikuwa amekasirika sana na akamuua Habili .



3.7 “Wapi ndugu yako?” Mungu aliuliza Kaini. “Sijui,” Kaini akadanganya, “sitakiwi kumlinda yeye.”

3.8 Lakini Mungu alimjibu, “Ninajua umemuuwa, Habili sasa umelaaniwa na utakuwa fukara (maskini), ardhi haitakuzalia chochote.”

3.9 Kwa hivyo Kaini alifukuzwa akaenda mashariki ya Edeni. Hakuweza kuabudu Mungu wala kuona jamii yake tena alikuwa pekee yake .

3.10 Baadaye Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtoto wa kiume mwingine badala ya Habili, aliitwa Sethi na alikuwa mzuri.

Adamu na Hawa walipata watoto wengine wengi na Adamu aliishi miaka mia tisa na thelathini na akafa vile Mungu alikuwa amesema.

